

Kwanini nguo za waliomwua Stefano ziwekwe miguuni mwa Sauli?.

Swali: Kulikuwa na sababu gani habari za nguo za waliomwua Stefano kuandikwa katika biblia? (Matendo 7:58).

Jibu: Turejee...

Matendo 7:58 "wakamtoa nje ya mji, wakampiga kwa mawe. Nao mashahidi WAKAWEKA NGUO ZAO MIGUUNI PA KIJANA MMOJA ALIYEITWA SAULI.

59 Wakampiga kwa mawe Stefano, naye akiomba, akisema, Bwana Yesu, pokea roho yangu".

Zipo tafiti zinasema kuwa zamani za biblia, akipatikana mtu na kosa la kustahili kuuawa kwa kupigwa mawe, basi wale mashahidi waliolishuhudia kosa la huyo mtu, kabla ya kutekeleza mauaji walivua nguo zao kama ishara ya kiapo walichokitoa/ushahidi kuwa ni kweli.

Lakini dhana hiyo haina marejeo yoyote ya biblia, hivyo si ya kusadikika.

Lakini sababu pekee yenye kuleta maana ya mavazi ya mashahidi

Kwanini nguo za waliomwua Stefano ziwekwe miguuni mwa Sauli?.

kuwekwa miguuni mwa Sauli ni ili wawe wepesi katika kutekeleza zoezi hilo la mauaji.

Ni kawaida wana michezo au wapiganaji kupunguza mavazi yao kabla ya mchezo kuanza ili wawe wepesi, ndicho walichokifanya hawa mashahidi, walipunguza mavazi yao ya nje, na kumpatia kijana Sauli awahifadbie kwa muda na baadae wazichukue baada ya kumuua Stefano.

Na tunasoma Sauli (*ambaye baadaye ndiye aliyekuja kuwa Paulo*), alikubali kuwatunzia..

Matendo 22:20 “Na damu ya Stefano shahidi wako ilipomwagwa, mimi nami nilikuwa nikisimama karibu, nikikubali, na kuzitunza nguo zao waliomwua”.

Sasa ni kwanini Bwana MUNGU aruhusu mavazi ya wauaji yatunzwe na Sauli?.

Sababu kuu ni kwamba Bwana MUNGU alijua Sauli atakuja kugeuka baadaye na kuwa mtumishi wake kwa watu wa Mataifa.

Kwanini nguo za waliomwua Stefano ziwekwe miguuni mwa Sauli?.

Hivyo kitendo cha zile nguo kuwekwa miguuni mwa Sauli ni kuweka sababu baadae ya Wayahudi pamoja na wakristo waliopo Yerusalem kumkataa, ili aende kwa watu wa mataifa...

Kwani watakapokumbuka lile tendo la kushiriki kwake kumuua Stefano, wamkatae na kumwona hafai..

Kwanini nguo za waliomwua Stefano ziwekwe miguuni mwa Sauli?.

Matendo 22:17 "Ikawa nilipokwisha kurudi Yerusalem, nilipokuwa nikisali ndani ya hekalu, nikawa hali ya kuzimia roho,

18 nikamwona, naye akiniambia, Hima, utoke Yerusalem upesi, KWA SABABU HAWATAKUBALI USHUHUDA WAKO katika habari zangu.

19 Nami nikasema, Bwana, wanajua hao ya kuwa mimi nalikuwa nikiwafunga gerezani wale wanaokuamini na kuwapiga katika kila sinagogi.

20 Na damu ya Stefano shahidi wako ilipomwagwa, mimi nami nilikuwa nikisimama karibu, nikikubali, na kuzitunza nguo zao waliomwua.

21 Naye akiniambia, Enenda zako; KWA KUWA NITAKUTUMA UENDE MBALI KWA WATU WA MATAIFA".

Na utaona faida ya Paulo kuhubiri kwa watu wa Mataifa ndio mazao ya nyaraka zote za Paulo, ambazo mpaka leo zimekuwa msingi wa Neno la Mungu.

Kwanini nguo za waliomwua Stefano ziwekwe miguuni mwa Sauli?.

Tunachojifunza zaidi kuwa yapo makosa ambayo yalitokea zamani, na MUNGU aliyaruhusu yatokee kwasababu yamebeba kusudi kubwa mbeleni.

Makosa mengine yaliruhusiwa zamani ili yatuondolee viburi leo, mengine yaliruhusiwa ili tupate fursa njema leo, na mengine ni ushuhuda kwa wengine na maonyo kwa wengi e n.k

Hivyo kila jambo lina kusudi lake.

Bwana akubariki.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kwa mawasiliano: +255693036618 au +255789001312

Kwanini nguo za waliomwua Stefano ziwekwe miguuni mwa Sauli?.

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

**Maziara ni nini? Je! Na Tunaruhusiwa kuyajenga kwenye
makaburi yetu?**

**Ni sahihi kusema sikuitiwa kuhubiri ubatizo kama Paulo
alivyosema (1Wakorintho 1:17)?**

Nini maana ya “Heri kuchagua jina jema kuliko mali nyingi”?

ANTIPA SHAHIDI WANGU, MWAMINIFU WANGU.

MWOMBENI BWANA WA MAVUNO APELEKE WATENDA KAZI.

Rudi Nyumbani

Share on:

WhatsApp